**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
**WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA**

# TANGAZO

## UUZAJI WA MITI YA MISAJI KWA NJIA YA MNADA WA KIELEKTRONIKI

Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) utauza miti aina ya misaji yenye jumla ya meta za ujazo **16,041.047** iliyopo katika Shamba la miti Longuza, Muheza Mkoani Tanga na Shamba la miti Mtibwa lililopo Turiani Mkoani Mororgoro. Jumla ya meta za ujazo **6,551.997** na **9,489.050** zitauzwa katika Shamba la miti Longuza na Mtibwa mtawalia.

1. Miti ya Misaji itauzwa kwa njia ya mnada wa kielektroniki kwa kuzingatia Kanuni ya 31 (ii) ya Kanuni za Misitu za Mwaka 2004. Mnada huu utafanyika siku ya **Alhamisi** tarehe **10 Septemba, 2026** kuanzia saa mbili kamili (02:00) asubuhi hadi saa nane na dakika kumi (08:10) mchana kwa Shamba la miti Longuza na **Ijumaa** tarehe **11 Septemba, 2026** kuanzia saa mbili kamili (02:00) asubuhi hadi saa saba na dakika nane (07:08) mchana kwa Shamba la miti Mtibwa.
2. Ili kushiriki kwenye mnada, mshiriki atajisajili kupitia anuani ifuatayo https://emisitu.tfs.go.tz kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi saa tisa kamili (9:00) mchana siku ya **Jumanne** ya tarehe **08 Septemba, 2026.** Kwa msaada wa usajili, wasiliana na: +255 766 356 149 au +255 766 857 062.
3. Washiriki wanakaribishwa kukagua miti iliyopo shambani wakati wa saa za kazi; kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu. Ukaguzi huo utafanyika kuanzia tarehe ya Tangazo hili hadi tarehe **08 Septemba, 2026** siku ya **Jumanne**. Wahifadhi wakuu au wasaidizi wao wa Shamba husika watakuwepo kwa ajili ya kutoa maelezo ya ziada.

**Masharti ya kushiriki Mnada huu**
Mshiriki lazima ajisajili na athibitishe ushiriki wake, na kwa kufanya hivyo, atakuwa amekubaliana na masharti yafuatayo: -

1. Mshiriki anapaswa kujisajili na kuthibitisha ushiriki wake kupitia https://emisitu.tfs.go.tz;
2. Kila Ploti itanadiwa peke yake kulingana na bei na ujazo uliopo,
3. Baada ya kukamilisha usajili, mshiriki atatakiwa kuthibitisha ushiriki wake angalau dakika tano (5) ambayo ni saa 01:55 asubuhi kabla ya muda wa mnada kuanza,
   **Muhimu**: Uthibitisho baada ya mnada kuanza hautakubaliwa.
4. Malipo yote yafanyike kupitia benki au mitandao ya watoa huduma za kifedha

baada ya kupokea hati ya madai (bill) ya Mfumo wa Makusanyo ya Serikali (GePG) itakayopatikana kwenye akaunti ya mshiriki kwenye mfumo wa mnada wa kielektroniki,

5. Mshiriki atakayeshinda atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25 %) ya thamani yote ya ununuzi ndani ya siku tatu (3) za kazi baada ya siku ya mnada. Fedha hizo hazitarudishwa endapo mshindi atashindwa kulipia ujazo aliouziwa. Mnunuzi ataruhusiwa kulipia zaidi ya asilimia 25 ya malipo ya kitalu chochote mara tu baada ya kukamilisha malipo ya awali ya 25% kwa vitalu vyote alivyonunua. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia siku ya mnada,
6. Mshiriki atakayefanikiwa kununua miti ya misaji hataruhusiwa kusafirisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa kanuni ya 50 (1) ya kanuni za misitu za mwaka 2004,
7. Mshiriki aliyefanikiwa atapaswa kuwasilisha kwa Mhifadhi wa shamba kielelezo cha kiasi cha fedha kilichowekwa, ndani ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.
8. Mshiriki aliyeshinda mnada atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya siku sitini (60) baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100. Aidha, endapo kutajitokeza changamoto ambazo zitasababisha kushindwa kuondoa mazao hayo ya misitu kwa muda uliopangwa, barua rasmi iwasilishwe kumjulisha Mhifadhi Mkuu wa Shamba kwa maamuzi,
9. Miti hiyo ya misaji itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo kufanyika.

**Wajibu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania;**

1. Kupanga viunga vya kuuza kama vinavyooneshwa katika Jedwali la orodha ya bei za kianzio (mrabaha tu) kwa mita moja ya ujazo, na
2. Kutoa barua za ushindi na hati za madai kwa wanunuzi walioshinda mnada kwa kila ploti mara baada ya kumalizika kwa mnada.

**Viunga vya Miti ya Misaji inayouzwa**

Ploti zimepangwa kwa mafungu, ambapo kila baada ya saa moja fungu moja litauzwa. Vilevile ndani ya muda wa mnada uliotengwa kutakuwa na mapumziko (waterbreak) ya dakika mbili kila baada ya fungu moja kuuzwa.

***NB**: Muda wa ziada wa saa moja utatolewa kwa ajili ya kuuza viunga vyote ambavyo havikuuzwa ndani ya muda rasmi wa mnada uliopangwa.*

Viunga vinavyouzwa vimeorodheshwa katika jedwali namba 1 na jedwali namba 2 kama ifuatavyo: -

**JEDWALI NA. 1: VIUNGA VITAKAVYOUZWA KATIKA SHAMBA LA MITI LONGUZA SIKU YA ALHAMISI TAREHE 10 SEPTEMBA, 2026**

| NA. | Jina la Kiunga | Ujazo kwa kila Kiunga ($M^3$) | Bei ya Kuanzia Kwa meta moja ya ujazo (TZS/ $M^3$) | Fungu Litakalouzwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KH2-P7 | 148.064 | 850,000.00 | Fungu Na.1<br><br>Muda; saa moja (1)<br>Kuanzia saa 02:00 - 03:00 Asubuhi |
| 2 | KH2-P9 | 158.310 | 850,000.00 | |
| 3 | KH2-P24 | 294.084 | 850,000.00 | |
| 4 | KH2-P40 | 119.134 | 850,000.00 | |
| 5 | KH2-P41 | 114.389 | 850,000.00 | |
| 6 | KH3-P50 | 315.720 | 850,000.00 | |
| 7 | KH3-P55 | 204.857 | 850,000.00 | Fungu Na.2<br><br>Muda; saa moja (1)<br>Kuanzia saa 03:02 - 04:02 Asubuhi |
| 8 | LG11-1 | 179.816 | 850,000.00 | |
| 9 | LG11-2 | 110.791 | 850,000.00 | |
| 10 | LG11-3 | 117.419 | 850,000.00 | |
| 11 | LG11-4 | 119.787 | 850,000.00 | |
| 12 | LG11-5 | 170.547 | 850,000.00 | |
| 13 | LG11-29 | 296.485 | 850,000.00 | |
| 14 | LG11-30 | 241.065 | 850,000.00 | Fungu Na.3<br><br>Muda; saa moja (1)<br>Kuanzia saa 04:04 - 05:04 Asubuhi |
| 15 | LG11-31 | 199.806 | 850,000.00 | |
| 16 | LG11-32 | 240.333 | 850,000.00 | |
| 17 | LG11-6 | 115.300 | 850,000.00 | |
| 18 | LG11-7 | 87.829 | 850,000.00 | |
| 19 | LG11-8 | 82.542 | 850,000.00 | |
| 20 | LG11-9 | 100.112 | 850,000.00 | |
| 21 | LG11-10 | 191.873 | 850,000.00 | Fungu Na.4<br><br>Muda; saa moja (1)<br>Kuanzia saa 05:06 - 06:06 Mchana |
| 22 | LG11-11 | 95.970 | 850,000.00 | |
| 23 | LG11-12 | 90.825 | 850,000.00 | |
| 24 | LG11-13 | 116.518 | 850,000.00 | |
| 25 | LG11-14 | 182.965 | 850,000.00 | |
| 26 | LG11-15 | 133.558 | 850,000.00 | |
| 27 | LG11-16 | 148.505 | 850,000.00 | Fungu Na.5<br><br>Muda; saa moja (1)<br>Kuanzia saa 06:08 - 07:08 Mchana |
| 28 | LG11-17 | 131.870 | 850,000.00 | |
| 29 | LG11-18 | 175.588 | 850,000.00 | |
| 30 | LG11-19 | 267.311 | 850,000.00 | |
| 31 | LG11-20 | 183.198 | 850,000.00 | |
| 32 | LG11-21 | 142.882 | 850,000.00 | |
| 33 | LG11-22 | 158.556 | 850,000.00 | Fungu Na.6<br><br>Muda; saa moja (1)<br>Kuanzia saa 07:10 - 08:10 Mchana |
| 34 | LG11-23 | 183.681 | 850,000.00 | |
| 35 | LG11-24 | 187.881 | 850,000.00 | |
| 36 | LG11-25 | 111.916 | 850,000.00 | |
| 37 | LG11-26 | 324.338 | 850,000.00 | |
| 38 | LG11-27 | 149.295 | 850,000.00 | |
| 39 | LG11-28 | 158.877 | 850,000.00 | |
| | **JUMLA** | **6,551.997** | | |

**JEDWALI Na. 2: VIUNGA VITAKAVYOUZWA KATIKA SHAMBA LA MITI MTIBWA SIKU YA IJUMAA TAREHE 11 SEPTEMBA, 2026**

| NA. | Jina la Kiunga | Ujazo kwa kila Kiunga ($M^3$) | Bei ya Kuanzia Kwa meta moja ya ujazo (TZS/ $M^3$) | Fungu Litakalouzwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | LR15C | 268.410 | 250,000 | Fungu Na.1 Muda; saa moja (1) Kuanzia saa 02:00 - 03:00 Asubuhi |
| 2 | LR18-20 | 368.870 | 420,000 | |
| 3 | LR15G | 270.380 | 250,000 | |
| 4 | LR18-21 | 342.210 | 420,000 | |
| 5 | LR21-1 | 177.030 | 400,000 | |
| 6 | LR18-16 | 324.720 | 420,000 | |
| 7 | LR18-19 | 503.360 | 400,000 | Fungu Na.2 Muda; saa moja (1) Kuanzia saa 03:02 - 04:02 Asubuhi |
| 8 | LR15E | 244.430 | 220,000 | |
| 9 | LR17-19 | 494.070 | 400,000 | |
| 10 | LR21-3 | 203.310 | 400,000 | |
| 11 | LR21-5 | 272.180 | 400,000 | |
| 12 | LR18-24 | 447.230 | 420,000 | |
| 13 | LR18-25 | 496.520 | 420,000 | Fungu Na.3 Muda; saa moja (1) Kuanzia saa 04:04 - 05:04 Asubuhi |
| 14 | LR21-6 | 186.580 | 400,000 | |
| 15 | LR17-15 | 223.140 | 420,000 | |
| 16 | LR15M | 222.650 | 200,000 | |
| 17 | LR17-20 | 356.390 | 400,000 | |
| 18 | LR17-21 | 166.620 | 400,000 | |
| 19 | LR21-8 | 191.910 | 350,000 | Fungu Na.4 Muda; saa moja (1) Kuanzia saa 05:06 - 06:06 Mchana |
| 20 | LR17-23 | 465.660 | 400,000 | |
| 21 | LR17-24 | 431.510 | 400,000 | |
| 22 | LR21-2 | 338.630 | 370,000 | |
| 23 | LR18-22 | 468.980 | 420,000 | |
| 24 | LR21-7 | 209.350 | 350,000 | |
| 25 | LR21-4 | 239.190 | 400,000 | Fungu Na.5 Muda; saa moja (1) Kuanzia saa 06:08 - 07:08 Mchana |
| 26 | LR18-27 | 315.460 | 400,000 | |
| 27 | LR18-23 | 437.900 | 420,000 | |
| 28 | LR17-22 | 481.820 | 400,000 | |
| 29 | LR15N | 340.540 | 250,000 | |
| **JUMLA** | | **9,489.050** | | |

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya: www.tfs.go.tz

Limetolewa na;

**KAMISHNA WA UHIFADHI**
**S. L. P. 2228,**
**DODOMA.**